Mpango wa Huduma ya Taifa ya Afya [NHS] wa Chanjo ya kukinga Kovid-19 - Norfolk na Waveney

Habari hii ni sahihi kuanzia tarehe 10 Februari 2021

Tunaandika kwa jamii wote ili kutoa habari na uhakikisho kwa wagonjwa, jamii na jamaa, na watunza wasaidizi kote Norfolk na Waveney kuhusu mpango wa chanjo ya Kovid-19

Ikiwa unastahiki kupata chanjo, tafadhali kuwa na subira, tutawasiliana na wewe na kukutolea miadi ya chanjo.

USHAURI KWA UJUMLA: Tafadhali usianze mawasiliano na daktari wako kuhusu chanjo. Utapata miadi ya chanjo wakati wako upofika. Itatuchukua wiki chache tu kabla kuweza kuwasiliana na kila mtu.

Mtu yeyote mwenye umri wa miaka 70+, au ambaye ametambuliwa na **Huduma ya kitaifa ya afya [NHS] kuwa** anayeweza kuathirika kwa jinsi ya hali yake ya afya, na pia ni ambaye bado hajapewa miadi, anapaswa kuwasiliana na kituo cha miandi cha huduma cha afya cha kitaifa akitumia:

1. **Mtandaoni** - www.nhs.uk/covid-vaccination
2. **Kwa simu** - piga simu **119** (ya bure), kati ya saa moja asubuhi na saa tano za usiku katika siku zote saba za wiki.

Tafadhali tumia njia hizo za kwanzisha mawasiliano. Lakini ikiwa nafasi inaoyokufaa haitapatikani, watu wanaweza pia kupiga simu katika vituo vya daktari waliyejisajilisha naye.

Jinsi, na ni lini utapata miadi yako ya chanjo

Huduma ya Afya ya kitaifa inakusanya orodha ya watu walio katika vikundi vya watu walio katika kipaumbele cha kwanza chanjo. Vikundi hivi vya kipaumbele ni kama:

- wale wenye umri wa miaka 80 na zaidi
- wale walio na zaidi ya miaka 75
- wale wenye umri zaidi ya miaka 70
- mtu yeyote anayeishi katika nyumba ya utunzaji wa watu wazima wakubwa (mwenye umri wa miaka 65+)
- wahudumu wa nyumbani (zaidi ya miaka 65)
- wahudumu wa mstali wa mbele wa huduma za afya
- wafanyikazi wa mstali wa mbele wa huduma za jamii
- watu wazima katika orodha ya wagonjwa wanaokingwa na huduma ya afya ya taifa [NHS], na wanaoishi katika mazingira magumu.

Chanjo hutolewa kwa njia ya kuteuliwa tu kwa watu katika vikundi vya kipaumbele kama hapo juu. Ikiwa bado haujaalikwa kufanya miadi, watawasiliana na wewe kwa njia moja au nyingine katika siku za wiki zijazo wakipitia:

- Utapokea mwaliko kwa barua, simu au maandishi kutoka kwa daktari wa eneo lako, ili upange miadi katika kituo cha daktari huo na ili kuwapa chanjo watu waliosajiliwa naye, na pia kwa watu wengine kutoka vituo vingine vya madaktari walio jirani.
- Barua kutoka kwa huduma ya afya ya taifa la England [NHS England], itakualika kufanya miadi katika kituo cha hospitali, duka la jamii la dawa, au katika kituo kikubwa cha chanjo kupitia wavuti wa kitaifa au kwa simu.

Mtu yeyote ambaye ana mahitaji ya usaidizi wa mwendo, ufikiaji, au shida yoyote ya kufika kwa miadi ya chanjo anapaswa kujadili jambo hilo wakati wanapowasiliana kupanga miadi. Msaada kutoka kwa huduma anuwai za uchukuzi wa jamii unapatikana kwa watu wanaostahiki.

Ambapo utapata chanjo zako

Unapopatiwa miadi au kualikwa kupanga, tafadhali tenda kwa haraka na usicheleweshe. Kulingana na idadi ya watu wengi tutakaoweza kuchanja haraka katika kipimo cha kwanza, ndivyo jamii zetu, marafiki na familia watakavyolindwa kutoka kwa ugonjwa wa KOVID-19.

Kuna aina nne za maeneo ya chanjo ambayo watu wanaostahiki wanapewa kwa sasa huko Norfolk na Waveney:

- maeneo ya chanjo yanayoongozwa na Waganga [GPs]
- Vituo vitatu vya chanjo ya hospitali: Norfolk na Norwich, James Paget na hospitali za Queen Elizabeth
- Vituo vikubwa vya chanjo ni pamoja na Castle Quarter huko Norwich, Kings Lynn Corn Exchange, Connaught Hall huko Attleborough na Kituo cha Jamii cha North Walsham.
- Mkemia wa Hayden huko Lowestoft - pamoja na maduka ya jamii ya madawa mengine yanayotoa chanjo kwa wiki zijazo

Unaweza kupewa fursa ya kuchagua kituo, au unaweza kupewa miadi kwenye kituo maalum. Vituo vyote vina mahali ya kuweka magali na ni ya kufikika kwa urahisi.

Habari kuhusu kuhudhuria miadi ya chanjo

Tafadhali hakikisha unapohudhuria miadi zote ulizopewa - kwa kipimo chako cha mwanzo na cha pili. Hizi kwa kawaida huwa ni baada wiki 12. Lazima uhudhurie miadi zote mbili ili kuhakikisha kuwa umepata kinga dhidi ya KOVID-19 inayotakikana.

Hutapata kinga kamili ya chanjo hadi karibu wiki tatu baada ya kipimo chako cha pili.

Unapohudhuria chanjo yako:

- Tafadhali usifike zaidi ya dakika 5-10 kabla ya muda wako wa miadi. Kwa sababu ikiwa unafanya hivyo, watu lazima wafanye foleni kwa muda mrefu na hii itaweza kusababibisha ugumu wa utekelezaji wa umbali wa utekutengano kwa jamii.
- Uwe na nambari yako ya huduma ya afya ya kitaifa [NHS], au barua ya mwaliko. Nambari yako ya huduma ya afya ya kitaifa inawezapatikana kwenye hati au barua anuwai za huduma ya taifa ya afaya [NHS] ambazo unaweza kuwa umepokea, kuhusu huduma yako ya afya au dawa. **Tafadhali usimpigie daktari wako simu**

kwa ajili ya kumuliza nambari yako ya kusajiliwa na huduma ya afya ya taifa, kwa sababu laini zao za simu zinatumika kwa shughuli nyingi sana, na zinapaswa kuwekwa wazi kwa wagonjwa ambao wanahitaji kupanga miadi.

- Ikiwa unatumia dawa ya kuzuia ujazo wa damu (dawa ya kupunguza uzito wa damu kama vile warfarin) tafadhali chukua 'kitabu chako cha rangi ya manjano' kwenye miadi yako ya chanjo. Utaweza kupokea chanjo ikiwa umesasisha upimaji uliopangwa wa uwiano wa kawaida wa kimataifa. [INR]
- Uwiano wa kawaida wa kimataifa [INR] na matokeo yako ya mwisho yalikuwa chini ya kikomo cha juu cha anuwai yako ya INR.
- Tafadhali vaa mavazi ilio ina urahisi wakufikia mkono wa juu. Inapendekezwa uvae fulana ya mikono mfupi kama safu yako, chini ya nguo. Lakini tafadhali pia vaa mavaazi ya kuzuia baridi na tabaka kadhaa nguo na koti ili kukingana na hali ya hewa ya baridi, kabla na baada ya chanjo yako.
- Ikiwa una uwoga au hupendi sindano, basi julisha mtu anayekupa chanjo yako ili ajue vile anavyoweza kukusaidia.
- Kumbuka vaa kifuniko cha mapua na kinyua wakati unaposafiri kwelekea mahali popote, unapotoka nyumbani na pia wakati wa miadi yako, tena chukua hatua ya kudumisha utengano wa kijamii wakati wote. Unapaswa pia kunawa au kusafisha mikono yako kabla na baadaye.
- Tafadhali waheshimu wafanyikazi wetu. Wanafanya kazi masaa marefu, jioni na wikendi kuwapa watu chanjo. Matusi au ugomvi kwa wafanyikazi wa huduma ya afya ya taifa [NHS] au kwa wasaidizi wa wakujitolea, hautakubaliwa na maafisa wa polisi wanaunga mkono na wanahakikisha usalama kwa kila mtu katika eneo zetu zote za chanjo.

Hata kama umepokea chanjo yako ya Kovid-19 ya mwanzo au iwe ni ya pili, kila mtu anapaswa kuendelea kufuata mwongozo wote wa kudhibiti virusi na kuokoa maisha. Hii inamaanisha kukaa nyumbani kwa kadri inavyowezekana na kufuata mwongozo uliotolewa na serikali, kwa kunawa mikono kila wakati, kufunika mapua ma kinyua, kudumisha utengano wa kijamii wakati wote ikiwa ni lazima utoke nnje.

Kuendelea kupokea habari na mpango wa chanjo ya Covid-19 katika eneo lako

NHS Norfolk na Waveney CCG wana ukurasa kujitolea kwa wa wavuti wa habari ya kisasa kuhusu mpango wa chanjo ya Covid-19: https://www.norfolkandwaveneyccg.nhs.uk/covid-19-vaccination-programme

Habari ya wavuti huu unaweza kubadilishwa kuwa lugha unayozungumza na:



Kubonyeza kitufe cha 'Ongea'
[Clicking on the ‘Speak’ button]

Kisha kuchagua kitufe cha 'Ulimwengu'

Kisha chagua lugha unayozungumza kutoka kwenye orodha inayoonekana